# HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. MKUU WA MKOA WA SHINYANGA Mhe. MBONI MHITA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAZEE DUNIANI KIMKOA YANAYOFANYIKIA KIJIJI CHA JOMU, KATA YA TINDE HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA TAREHE 23 SEPTEMBA,2025

**Katibu Tawala Mkoa,**

**Kamati ya Usalama Mkoa**

**Kamati ya usalama Wilaya ya Shinyanga,**

**Mh. Mwenyekiti wa CCM Mkoa,**

**Mhe. Mkuu wa Wilaya Shinyanga,**

**Mkurugenzi Mtendaji Shinyanga DC,**

**Katibu Tawala Wilaya ya Shinyanga,**

**Wakuu wa Sehemu, Vitengo na Wataalam toka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga**

**Afisa Tarafa Itwangi,**

**Wakuu wa Idara na wataalamu toka Halmashauri zote 6**

**Mwenyekiti Baraza la Wazee Mkoa,**

**Mwenyekiti Baraza la Wazee la CCM Mkoa,**

**Viongozi wa Mabaraza ya Wazee Mkoa na Halmashauri zote 6,**

**Mtendaji wa Kata ya Tinde,**

**Mtendaji na Mwenyekiti wa Kijiji cha Jomu,**

**Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji Kituli, Ngokolo, Nhumbili, Nshishinulu,**

**Mwenyekiti Umoja wa Wanaume Mkoa,**

**Mwenyekiti Umoja wa Wastaafu Tanzania Mkoa wa Shinyanga**

**Mwenyekiti SHIVYWATA Mkoa**

**Wadau na Taasisi zinazoshughulika na utoaji huduma kwa Wazee.**

**Wazee wote,**

**Viongozi wa Dini,**

**Waandishi wa habari,**

**Waalikwa wote**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kazi Iendelee**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kufika hapa pamoja nami kuwa nanyi leo nikiwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya ya siku ya Wazee Dunani ambayo Kimkoa yanafanyikia Halmashauri ya Wilaya ya Shnyanga. Kwa moyo wa dhati napenda kuwashukuru wote kwa kufika kwenu.

**Mabibi na Mabwana,**

Sote tunatambua Wazee ni watu maalumu ambao tunawategemea kwa mawazo, hekima na busara zao kwa maendeleo ya Taifa na jamii kwa ujumla.

**Mabibi na Mabwana,**

Nipende kupongeza wote walioshiriki katika maandalizi ya maadhimisho haya ikiwemo Sekretariati ya Mkoa wa Shinyanga, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Baraza la Wazee Mkoa na Baraza la wazee la

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Viongozi na Watendaji wote Kata ya Tinde na Kijiji cha Jomu, wanajamii wote wa Kata ya Tinde.

**Mabibi na Mabwana,**
Kama tunavyofahamu kila mwaka tarehe 1 ya mwezi Oktoba huadhimishwa siku ya Kimataifa ya Wazee duniani kwa lengo kuu la jamii kuhabarishwa na kuelimishwa juu ya umuhimu wa wazee, kutumia hekima na busara walizonazo, kuwaheshimu, kuwatunza, na kuwajali, Wazee kuonyesha uwezo walionao katika shughuli mbalimbali wanazofanya.

Kwa mwaka huu maadhimisho ya Kitaifa yanafanyikia Mkoa a Ruvuma na ya Kimkoa yanafanyika katika Halmashauri ya Wilaya Shinyanga, Kata ya Tinde Kijiji cha Jomu.

**Mabibi na Mabwana,**
Kauli mbiu ya mwaka huu ya maadhimisho haya inasema “**Wazee Tushiriki Uchaguzi Kwa Ustawi wa Jamii Yetu”**

**”.** Sote tunatambua tupo katika mwaka wa uchaguzi wa Viongozi katika ngazi zote. Ni haki ya kila Mtanzania mwenye sifa za kupiga kura basi kushiriki katika uchaguzi. Aidha wazee ni hazina na ni haki ya msingi ya kikatiba ya kila mzee kushiriki katika uchaguzi. Hivyo niwaombe wazee wote wa Mkoa wa Shinyanga kushiriki katika uchaguzi na kwenda kupiga kura tarhe 29/10/2025 kwa maendeleo na ustawi wa wazee,jamii na Taifa kwa ujumla.

**Mabibi na Mabwana,**
Mkoa wetu wa Shinyanga unaendelea kutekeleza maelekezo mbalimbali yanayotolewa juu ya utoaji wa huduma bora kwa Wazee kupitia pia miongozo na Sera mbalimbali zilizopo ikiwemo Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 Tolea la II la mwaka 2024.

Aidha niyapongeze mabaraza ya Wazee ngazi zote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutetea haki na maslahi ya Wazee. Niendelee kuzielekeza Halmashauri zote 6 kuendelea kushirikiana na Mabaraza haya pamoja na Taasisi na wadau wote wanaotekeleza shughuli za wazee katika maneo yenu pamoja na kutetea masuala ya wazee katika jamii ikiwemo Umoja wa Wanaume pamoja na Umoja wa Wazee Wastaafu Tz.

Nawaagiza pia Wakurugenzi wote wa Halmashauri zote 6 kuhakikisha wanayasimamia na kuyawezesha mabaraza ya wazee ili yaweze kufanya kazi yake kikamilifu lakini pia kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za wazee pamoja na kuwashirikisha wawakilishi wa mabaraza ya wazee katika mikutano na vikao vya maamuzi vya Halmashauri.

**Mabibi na Mabwana,**
Kwa mujibu wa takwimu za sense ya watu na makazi ya mwaka 2022 inaonyesha Mkoa wa Shinyanga unao Wazee 100,626. Kati ya Wazee hao waliopatiwa kadi za matibabu bila malipo ni 43256 sawa na asilimia 43 na waliopatiwa kadi za CHF ni 11063 sawa na asilimia 11. Nizipongeze Halmashauri ambazo zimetoa kadi za matibabu bila malipo kwa wazee pamoja nakadi za CHF

kwa kufanya hivi inasaidia wazee wetu kuwa na uhakika wa matibabu katika vituo vyetu.

**Mabibi na Mabwana,**
Serikali yetu imeboresha miundombinu na huduma za afya kwa kujenga vituo vya afya na Hospitali za Wilaya pamoja na kuboresha Zahanati, serikali pia kwa kutambua thamani ya wazee katika upatikanaji wa huduma za afya katika Hospitali za Mkoa na Wilaya kuna vyumba maalum kwa ajili ya kutolea huduma za matibabu kwa wazee na vituo ambavyo kutokana na changamoto ya miundo mbinu na watumishi imekuwa ikizingatia kutoa kipaumbele katika utoaji wa huduma kwa wazee kwanza ikiwemo kuweka mabango yanayoelekeza ***MPISHE MZEE APATE HUDUMA KWANZA.***

Changamoto ya ukosefu wa dawa naagiza kila Halmashauri kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa dawa na fedha katika vituo vyetu kwa kila robo, kuagiza dawa na vifaa tiba kwa wakati kwa mujibu wa mzunguko wa uagizaji pamoja na kuhakikisha makundi ya msamaha yanatengewa dawa zao ili kuepusha usumbufu wa mzee kukosa dawa

**Mabibi na mabwana,**
Kama tunavyofahamu tunao wajibu wa kuhakikisha wazee wanatunzwa na kutonyanyaswa kwa jinsi yeyote kama sera ya Taifa ya Wazee inavyotuelekeza, lakini bado tunaona kuna baadhi ya wazee wamekuwa wakitelekezwa na familia zao na hata kuachiwa mzigo mkubwa wa kulea wajukuu kitu ambacho kimepelekea wazee hawa kuishi maisha ya shida na magumu, pia wapo wazee ambao wamekuwa wakibaguliwa, kutothaminiwa na

kutelekezwa kutokana na jamii kuwa na imani potofu za uchawi kwa wazee.

**Mabibi na Mabwana,**

Tukumbuke kuwa kadri umri unavyoongezeka ndivyo baadhi ya viungo navyo huzeeka lakini maumbile na ngozi kusinyaa lakini pia kukumbwa na magonjwa nyemelezi mara kwa mara, hivyo kipindi hiki mzee anahitaji sana upendo, kutunzwa na kuthaminiwa ili aweze kuishi kwa amani na furaha na sio kufanyiwa vitendo vya kikatili.

Nitoe rai kwa jamii hususan vijana kuwatunza wazee wao na kutowanyanyasa wazee kutokana na uzee wao kwani sote tunaelekea huko hivyo lazima tubadilike na kuwa na kizazi bora chenye kuwajali wazee kwani **UZEE NI HAZINA,** pia naziagiza kamati za usalama ngazi zote kuhakikisha ulinzi na usalama wa wazee unazingatiwa na yeyote atakayefanya ukatili kwa mzee na kwa mtu yeyote basi achukuliwe hatua kali za kisheria.

Aidha sote kwa pamoja tuendelee kutoa elimu ya haki za wazee, malezi na matunzo kwa wazee wetu pamoja na elimu ya kiafya kwani wazee nao wanakumbana na magonjwa yanayoambukiza kama VVU na ukimwi pamoja na magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari, magonjwa ya moyo ambayo huwapata zaidi wazee.

Niwaombe sana Wazee na wanajamii kwa ujumla kuendelea kujitokeza katika kupata elimu mbalimbali ya afya na upimaji wa afya zetu katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya na kupitia huduma mkoba kwani kinga ni bora. Aidha naagiza Halmashauri zote 6 kuhakikisha wanawafikia Wazee na wanajamii walio pembezoni na vituo vyetu kwa njia ya huduma

mkoba (outreach services) ili wapate elimu na huduma mbalimbal za afya.

Aidha tuendelee kutokomeza matukio ya ukatili yanavyofanyiwa wazee wetu na kuondoa imani potofu pamoja na kutoa taarifa kwa wanaofanya unyanyasaji na ukatili kwa wazee pamoja na wale wanaojihusisha na ramli chonganishi zinazoongeza ukatili katika jamii ili waweze kufikishwa katika vyombo vya sheria na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.Halmashauri ziendelee kutoa elimu ya ujasiriamali na uundaji wa vikundi ili wazee wanawake waweze kupata mikopo isiyo na riba kupitia asilimia 4 ya fedha za mapato ya ndani.

Wazee tuendelee kutumia busara na hekima tulizonazo kutoa nasaha zetu kwa vijana, familia na jamii kwa ujumla ili kuondoa wimbi la mmomonyoko wa maadili katika jamii ambao pia unachangia kuwepo na matukio ya ukatili wa kijinsia katika jamii.

**Mabibi na Mabwana,**
Ni imani yangu kupitia maadhimisho haya Wazee na wanajamii tutapata elimu ya afya na upimaji wa afya zetu kwani kinga ni bora zaidi kuliko tiba. Tuendelee kushirikiana katika kutoa hamasa na elimu kwa wenzetu ambao tumewaacha majumbani ili na wao wahamasike na kufika kwa wataalam na kupata elimu na kupata upimaji wa afya zao katika vituo vyetu vya kutolea huduma za afya na kupitia huduma mkoba. Tuendelee kuwatunza wazee wetu ili wazeeke kwa heshima kwani ni Baraka pia kwa Mungu.

Mwisho niwahimize wananchi wote wa Mkoa wa Shinyanga ifikapo tarehe 29/10/2025 twende kupige kura katika vituo vya kupigia kura kwani ni haki ya msingi kikatiba. Nitoe rai kuepuka matendo yanayoweza pelekea uvunjifu wa amani wakati wa na

baada ya uchaguzi. Sote kwa pamoja tuitunze amani ya Nchi yetu.

**Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania.**

**“Uzee na kuzeeka haukwepeki”**

***AHSANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA***